JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU
MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2019

Imetayarishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia Biashara
Haramu ya Dawa za Kulevya (Sura 95)

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2019

Imetayarishwa na
Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya,
S.L.P 80327,
8 Barabara ya Kivukoni Front,
11486 Dar es Salaam
Barua pepe:cg@dcea.go.tz
Tovuti: www.dcea.go.tz
Instagram: @dceatanzania
Twitter: dceatanzania
Facebook: dcea Tanzania

ISBN: 978-9987-9596-8-6

Imetayarishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya (Sura 95)

MATAMKO YA VIONGOZI KATIKA KUKABILIANA NA TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 (CCM) ya mwaka 2015-2020 ilitoa ahadi ya kuisimamia Serikali katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya nchini. Katika kutekeleza Ilani hiyo, viongozi wa kitaifa wamekuwa wakihamasisha jamii kupambana na tatizo la dawa za kulevya nchini kupitia njia mbalimbali yakiwemo matamko ambayo yamekuwa chachu ya mapambano. Yafuatayo ni matamko ya viongozi wa kitaifa katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya nchini:

MHESHIMIWA DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,

Dawa za kulevya zimekuwa ni janga kubwa kwa taifa letu na kundi linaloathirika zaidi ni vijana wa kiume na kike. Familia nyingi zimeathirika na nguvu kazi ya Taifa imepotea. Tutaushughulikia mtandao huo hususan wafanyabiashara wakubwa wanaojihusisha na dawa ya kulevya bila ajizi.

MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN
MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Dawa za kulevya zina athari kwa Taifa kwani huchangia kuwepo kwa mmomonyoko wa maadili na hudhoofisha nguvu kazi ya Taifa. Hivyo, jamii inapaswa kushiriki kikamilifu katika kupiga vita dawa za kulevya.

MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (Mb)
WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,

Serikali imeazimia kupambana vilivyo na wafanyabiashara wa dawa za kulevya na kuhakikisha tatizo la dawa hizi linakuwa historia Nchini. Tunaponadi uchumi wa viwanda lazima tuwe na nguvu kazi yenye siha njema kuweza kushiriki kwenye kazi halali za kujenga Taifa letu. Yeyote anayetaka kudhoofisha nguvu kazi ya Taifa letu au kuhujumu jitihada za uchumi wa viwanda atashughulikiwa bila huruma. Ni vyema wazazi, walezi na jamii kuwa karibu na vijana wetu na kufuatilia nyendo zao ili kuwaepusha kuingia kwenye mkumbo wa matumizi ya dawa za kulevya.

MHESHIMIWA JENISTA JOAKIM MHAGAMA (Mb)
WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU)

Vita dhidi ya dawa za kulevya ni yetu sote, hivyo tushirikiane kwa pamoja kuishinda. Tusipopambana na dawa za kulevya tutashindwa kuwashirikisha vijana katika kujenga uchumi wa Nchi yetu. Watanzania wote tuungane kwa pamoja, kuhakikisha tunaishinda vita hiyo.

BW. JAMES WILBERT KAJI
KAIMU KAMISHNA JENERALI WA MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Ni vyema watanzania wote kutambua kuwa tatizo la dawa za kulevya linahusisha nyanja mbalimbali. Hivyo, ushirikiano wa dhati baina ya wadau wa sekta mbalimbali ndani na nje ya nchi pamoja na jamii kwa ujumla unahitajika katika kukabiliana na tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Tushirikiane kuwafichua wauzaji wa dawa za kulevya na kuwapeleka kwenye tiba waraibu wa dawa hizo.

YALIYOMO

YALIYOMO i
ORODHA YA MAJEDWALI iii
ORODHA YA VIELELEZO iv
MAELEZO YA WAZIRI v
DIBAJI vi
FAHARASA vii
SURA YA KWANZA 1
1 TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI 1
1.1 Utangulizi 1
1.2 Matumizi na udhibiti wa dawa za kulevya duniani 1
1.3 Upunguzaji Madhara yanayosababishwa na Matumizi ya Dawa za Kulevya 7
1.4 Wanawake na matumizi ya dawa za kulevya 9
1.5 Wafungwa 9
SURA YA PILI 11
2 MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NCHINI 11
2.1 Utangulizi 11
2.1.1 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya 11
2.1.2 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya 11
2.1.3 Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya 11
2.1.4 Kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya 12
SURA YA TATU 13
3 KUPUNGUZA UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA 13
3.1 Utangulizi 13
3.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya 13
3.3 Uteketezaji wa Dawa za Kulevya 24
3.4 Kesi za Dawa za Kulevya 24
SURA YA NNE 26

4 KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA 26
4.1 Utangulizi 26
4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya 26
4.3 Sababu zinazochangia Matumizi ya Dawa za Kulevya. 26
4.4 Madhara ya Dawa za Kulevya 27
4.5 Kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya 30
SURA YA TANO 33
5 KUPUNGUZA MADHARA YANAYOTOKANA NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA 33
5.1 Utangulizi 33
5.2 Tiba ya Methadone 33
5.3 Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses) 35
SURA YA SITA 37
6 USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA KATIKA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA TANZANIA 37
6.1 Utangulizi 37
6.2 Ushirikiano wa Kimataifa 37
6.3 Ushirikiano wa Kikanda 38
6.4 Ushirikiano na Taasisi nyingine za Kimataifa 39
6.5 Ushirikiano wa Kitaifa 40
SURA YA SABA 41
7 CHANGAMOTO NA HATUA ZA BAADAYE 41
7.1 Utangulizi 41
7.2 Changamoto na hatua zilizochukuliwa 41
7.3 Mipango ya baadae 41

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2009-2019..14

Jedwali Na. 2: Idadi ya watuhumiwa wa Bangi na Mirungi waliokamatwa kati ya mwaka 2009-2019....16

Jedwali Na. 3: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2009-2019.18

Jedwali Na. 4: Idadi ya watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa nchini kati ya Mwaka 2009 - 2019....20

Jedwali Na. 5: Idadi ya waraibu waliohudumiwa na asasi za kiraia. 26

Jedwali Na. 6: Waraibu waliopata huduma katika nyumba za upataji nafuu kwa mwaka 2019…….. 28

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2009-2019. 15

Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2009-2019. 15

Kielelezo Na. 3: Mwenendo wa idadi ya watuhumiwa waliokamatwa kwa kujihusisha na Bangi na Mirungi nchini kati ya Mwaka 2009 – 2019.. 17

Kielelezo Na. 4: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2009-2019. 19

Kielelezo Na. 5: Idadi ya watuhumiwa waliokamatwa wakijihusisha na Heroin na Cocaine kati ya Mwaka 2009 - 2019.. 20

Kielelezo Na. 6: Mwenendo wa idadi ya watuhumiwa waliokamatwa wakijihusisha na Heroin na Cocaine kati ya Mwaka 2009 - 2019.. 21

MAELEZO YA WAZIRI

Tatizo la dawa za kulevya limeendelea kuikabili Nchi yetu na huathiri nyanja mbalimbali zikiwemo za kiafya, kiuchumi na mazingira. Mwaka 2019, Serikali ya awamu ya tano iliendelea kukabiliana na tatizo hilo kwa kufanya jitihada zinazolenga kupunguza upatikanaji na uhitajiwa dawa za kulevya, kupunguza madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa hizo pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Jitihada zilizofanyika ni pamoja na kufanya operesheni za ukamataji wa dawa za kulevya ambapo tani 21.16 za bangi, tani 9.07 za mirungi, kilo 55.35 za heroin na kilo 10.34 za cocaine zilikamatwa. Ukamataji wa dawa hizo uliwahusisha jumla ya watuhumiwa 10,384 na kesi zao zikiwa katika hatua mbalimbali mahakamani.

Katika kukabiliana na madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya ambapo hadi kufikia mwezi Desemba mwaka 2019, jumla ya waraibu 7,600 walipatiwa huduma za tiba ya dawa ya methadone katika vituo sita kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Dodoma. Pia, Serikali iliendelea kuratibu huduma za Upataji Nafuu kwa watumiaji wa dawa za kulevya ambapo waraibu wapatao 3,683 walipata huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses) zipatazo 20 na hivyo kufanya idadi ya waraibu waliohudumiwa kwa mwaka 2019 kufikia 11,283.

Aidha, elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya iliendelea kutolewa kwa umma kupitia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari, matukio ya kitaifa, semina, makongamano na mitandao ya kijamii, kama mkakati muhimu wa kupunguza matumizi haramu ya dawa za kulevya kwa makundi tofauti ya rika.

Serikali katika mwaka 2019 iliendelea kushirikiana na mataifa mengine na taasisi za kimataifa katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya. Mojawapo ya jitihada zilizofanyika ni pamoja na kubadilishana uzoefu, mafunzo na kupanga mikakati ya pamoja ya jinsi ya kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya. Nchi yetu imekuwa ikishiriki katika mikutano mbalimbali inayoratibiwa na Shirika la UNODC juu ya udhibiti wa dawa za kulevya. Ushirikiano huu na mataifa mengine na taasisi za kimataifa ulisaidia kupunguza uhalifu hasa katika ukanda wa bahari kuu ambako hapo awali ilikuwa ni njia kuu ya kupitishia dawa za kulevya na uhalifu mwingine wa kupangwa.

Nachukua nafasi hii kuwapongeza wadau wote, vikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama kwa ushirikiano uliowezesha udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika mwaka 2019. Pia nawapongeza wabunge kwa kukemea matumizi na biashara ya dawa za kulevya hivyo kuhamasisha jamii kukabiliana na tatizo hili ambalo ni hatari kwa mustakabali wa nchi yetu.

Napenda kuwahimiza wananchi wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali katika kupambana na tatizo la dawa za kulevya kwa manufaa yetu sote.

Jenista Joakim Mhagama (Mb)
Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu
(Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu)

DIBAJI

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya huandaliwa kila mwaka kwa mujibu wa kifungu cha 60 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015 ambacho kinaipa nguvu za kisheria Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuiandaa na kuiwasilisha Bungeni taarifa hiyo. Lengo la taarifa ya hali ya dawa za kulevya ni kuwawezesha wananchi kufahamu hali halisi ya tatizo la dawa za kulevya Nchini, jitihada zilizofanywa na Serikali kudhibiti tatizo hilo, mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizopo katika kudhibiti tatizo hilo.

Taarifa hii inatoa taswira ya tatizo la dawa za kulevya duniani pamoja na udhibiti wa tatizo hilo. Aidha, inafafanua mikakati ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya Nchini ambayo ni kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya, kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya, kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na ushirikiano wa kimataifa na kikanda katika udhibiti wa dawa za kulevya Nchini.

Taarifa inahitimisha kwa kuainisha changamoto zilizojitokeza katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini mwaka 2019. Aidha, mapendekezo na mipango ya baadaye ya kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya nchini imeorodheshwa.

Pamoja na masuala mengine taarifa hii inajumuisha shughuli mbalimbali zilizofanywa na wadau wa udhibiti wa dawa za kulevya wa ndani na nje ya nchi. Napenda niwashukuru wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine ikiwemo waliowasilisha taarifa zao ambazo zimesaidia kufanikisha uandaaji wa taarifa hii.

James Wilbert Kaji

KAIMU KAMISHNA JENERALI
MAMLAKA YA KUDHIBITI NA
KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA.

FAHARASA

ATS	Aphetamine Type Stimulants
BASATA	Baraza la Sanaa la Taifa
CDC	U.S Centers for Disease Control and Prevention
CND	The Commission on Narcotic Drugs
EU-ACT	European Union Action against Drugs and Organized Crime
GCLA	Government Chemist Laboratory Agency
GF	Global Fund
HONLEA	Heads of National Drug Law Enforcement Agencies
INCB	International Narcotics Control Board
MDH	Management and Development for Health
MSD	Medical Stores Department
NACP	National AIDS Control Project
NPS	National Prosecution Services
PPP	Public Private Partnership
TACAIDS	Tanzania Commisssion on AIDS
TMDA	Tanzania Medical and Drugs Authority
UNODC	United Nations Office on Drugs and Crime
UNAIDS	The Joint United Nations Programme on HIV and AIDS
VVU	Virusi vya UKIMWI

SURA YA KWANZA

1 TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI

1.1 Utangulizi

Sura hii imetumia dondoo za Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2019 katika kutoa picha ya tatizo la dawa za kulevya duniani. Sura hii inaonesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2019 tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya liliendelea kuiathiri dunia licha ya jitihada za udhibiti zilizofanyika. Katika kipindi hicho, dawa za kulevya zilizotumika zaidi ni bangi, dawa za kulevya jamii ya afyuni (heroin), metamphetamine, ecstasy, cocaine pamoja na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Aidha, katika kipindi hicho liliibuka tatizo la matumizi na biashara ya dawa mpya (New Psychotropic Substances) ambazo haziko kwenye orodha ya dawa zinazodhibitiwa (legal highs) chini ya mikataba ya kimataifa ya kudhibiti dawa za kulevya. Hata hivyo, jitihada ziliendelea kufanyika kudhibiti usambazaji wa dawa za kulevya pamoja na kutoa tiba kwa watumiaji wa dawa hizo.

1.2 Matumizi na udhibiti wa dawa za kulevya duniani

Idadi ya watu wanaotumia dawa za kulevya duniani iliongezeka kwa asilimia 30 katika muongo mmoja wa kuanzia mwaka 2009. Takwimu za mwaka 2017 zinaonesha kuwa watu milioni **271** ambao ni asilimia **5.5** ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 walitumia dawa za kulevya. Hali hii ilitokana na ongezeko la idadi ya watu na kuongezeka kwa uzalishaji wa dawa za kulevya duniani.

Bangi

Kulingana na takwimu za Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya Mwaka 2019, bangi ilitumiwa zaidi kuliko aina nyingine za dawa za kulevya ambapo takriban watu milioni **188** waliitumia dawa hiyo katika mwaka 2017. Ukamataji wa bangi eneo la Amerika ya Kaskazini ulipungua ikilinganishwa na miaka ya 2010 ambapo ukamataji ulikuwa asilimia **77** ya

ukamataji wa bangi yote duniani. Hatahivyo, bangi iliyokamatwa katika eneo hilo ni asilimia **21** ya bangi iliyokamatwa duniani katika kipindi cha mwaka 2017. Kwa upande wa Amerika ya Kusini, ukamataji uliendelea kufanyika na kufanikiwa kufikia asilimia 38 ya ukamataji wote wa bangi duniani katika kipindi cha mwaka 2017.

Dawa za kulevya jamii ya Afyuni

Dawa za kulevya jamii ya Afyuni ni dawa zilizopo katika kundi la vipumbaza (depressants) zinazotengenezwa kutokana na mmea wa afyuni (opium poppy) kwa kuchakatwa na kemikali bashirifu ili kuzalisha heroin na morphine (opiates). Aidha, dawa hizi aina ya afyuni zinaweza kutengenezwa katika maabara haramu kwa kuchanganya kemikali bashirifu pekee (opioids), kama vile fentanyl na tramadol. Inakadiriwa kuwa mwaka 2017 takriban watu milioni **53.4** duniani walitumia dawa za kulevya za jamii ya afyuni ambalo ni ongezeko la asilimia **56** ikilinganishwa na matumizi ya dawa hizo kwa mwaka 2016.

Afghanistan iliendelea kuongoza katika kilimo cha mimea ya afyuni ambapo katika mwaka 2018 ilizalisha asilimia **82** ya afyuni yote Duniani. Nchi nyingine zilizoongoza kwa kilimo cha mimea ya afyuni ni Myanmar kwa hekari **37,300** mwaka 2018 na Mexico hekari **30,600** katika kipindi cha mwaka 2016/17.

Tafiti zilizofanyika mwaka 2017, zilionesha kwamba Nigeria na India zilikuwa na idadi kubwa ya watumiaji wa dawa za kulevya za jamii ya afyuni na kusababisha idadi ya watumiaji duniani kupanda kutoka milioni **2.2** hadi milioni **6.1.** Aidha, Amerika ya Kaskazini imeathirika zaidi kwa matumizi ya afyuni za kutengenezwa (opioids) ambapo asilimia **4** ya watu wake walitumia dawa hizo katika mwaka 2017. Eneo la Mashariki ya Kati liliathirika zaidi kwa matumizi ya afyuni za aina ya opium, morphine na heroin (opiates) ambapo watumiaji walikuwa asilimia **1.6.** Asia ya Kusini ilikuwa na asilimia **35** ya watumiaji wa afyuni za kutengenezwa na ilizalisha nusu ya afyuni yote duniani. Inakadiriwa asilimia **35.5** ya watumiaji wa

dawa za kulevya wameathirika na dawa hizo kiasi cha kuhitaji tiba ikiwa ni ongezeko la asilimia **15** kutoka watu milioni **30.5** wa awali.

Ukamataji wa dawa za kulevya jamii ya afyuni (opiates) uliongezeka na kuvunja rekodi mwaka 2017 ambapo tani **693** za afyuni (opium) zilikamatwa, ikiwa ni ongezeko la asilimia tano zaidi ya ukamataji uliofanyika mwaka 2016. Aidha, tani **103** za heroin zilikamatwa ikiwa ni ongezeko la asilimia**13** zaidi ya ukamataji uliofanyika mwaka 2016 pamoja na tani **87** za morphine ikiwa ni ongezeko la asilimia **33.** Bara la Asia lilikabiliwa na tatizo kubwa la kilimo cha mimea ya afyuni (opium poppy) kwa kuzalisha asilimia **90** ya afyuni za asili (opiates) duniani. Pia, kiasi cha asilimia **85** ya afyuni iliyokamatwa duniani mwaka 2017 kilitoka kwenye Bara hilo. Hii inadhihirisha jitihada kubwa zilizofanywa na vyombo vya dola na kuimarika kwa ushirikiano wa kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya katika eneo hili.

Heroin

Heroin ni dawa ya kulevya aina ya afyuni inayozalishwa zaidi Afghanistan na husafirishwa kwenda maeneo mbalimbali duniani. Aidha, Nchi nyingine zinazozalisha heroin ni Mexico na Myanmar. Njia ya Balkan ambayo huanzia nchini Afghanistan, Iran, Uturuki hadi Ulaya imeendelea kuongoza katika biashara ya heroin ambapo, kiasi cha asilimia **47** ya heroin na morphine iliyokamatwa duniani nje ya Afghanistan mwaka 2017 ilikamatwa katika njia hii. Njia nyingine zinazotumika kusafirisha heroin kutoka Afghanistan ni njia ya kusini inayopitia Pakistan, Asia ya Kusini na Afrika na njia ya kaskazini kupitia Asia ya Kati hadi Urusi.

Kiasi kikubwa cha heroin inayokamatwa katika Amerika ya Kaskazini huzalishwa nchini Mexico. Kiasi kinachokamatwa kimekuwa kikiongezeka katika kipindi cha muongo mmoja kikihusisha heroin kutoka Mexico kuingia Marekani. Katika sampuli za heroin zilizochukuliwa mwaka 2016 nchini Marekani asilimia **80** ilithibitika kutokea nchi ya Mexico. Hatahivyo, heroin inayopatikana nchini Canada hutokea Afghanistan.

Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya

Dawa tiba zenye asili ya kulevya ni dawa zinazotumika kutibu maradhi mbalimbali lakini zinaweza kuleta ulevi iwapo zitatumika bila kufuata ushauri wa daktari. Kutokana na hatari hiyo dawa hizi zinatolewa kwa usimamizi maalum. Mfano wa dawa hizo ni pethidine, morphine, tramadol, fentanyl, ketamine, benzodiazepine, barbiturates na codeine. Takwimu halisi zinazoonesha chanzo cha dawa tiba zinazochepushwa kutoka vyanzo halali au kuzalishwa isivyo halali ni chache sana. Hatahivyo, kuna uwezekanao kuwa kiasi kikubwa cha dawa hizo zinazotumika kujistarehesha hasa fentanyl na tramadol huzalishwa isivyo halali kwenye maabara bubu na kiasi kidogo huchepushwa kutoka vyanzo halali. Tramadol huzalishwa katika nchi za Afrika ya Kaskazini na Mashariki ya Kati mahsusi kwa ajili ya ulevi ingawa hakuna takwimu za kutosha kudhihirisha hilo.

Tofauti na fentanyl na tramadol dawa tiba nyingine zenye asili ya kulevya zinaonekana kuchepushwa kutoka vyanzo halali hasa katika nchi zilizo nje ya Marekani. Kuna ushahidi wa uchepushaji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya codeine na oxycodone kutoka vyanzo halali ingawa uchepushaji huo ulikuwa wa kiasi kidogo. Hali hiyo inaweza kuwa inasababishwa na uwezo mdogo wa kutambua uchepushaji na kukosekana kwa mfumo thabiti wa utoaji taarifa za uchepushaji.

Katika kipindi cha miaka mitatu ukamataji wa tramadol duniani uliongezeka kutoka kilo **10** mwaka 2010 hadi tani tisa mwaka 2013. Mwaka 2017 ulivunja rekodi ya ukamataji wa tramadol ambapo tani **125** zilikamatwa. Takwimu za hivi karibuni zinaonesha kuwa nchi ya Nigeria ina tatizo kubwa kuliko ilivyokuwa inafahamika hapo awali, kwani asilimia **4.7** ya watu wenye umri wa miaka **15** hadi **64** walitumia dawa tiba zenye asili ya kulevya kama vilevi. Tramadol iliongoza katika matumizi mabaya ya dawa tiba zenye asili ya kulevya katika nchi hiyo.

Mwaka 2017, Amerika ya Kaskazini ilipata janga la vifo vipatavyo **47,000** vilivyotokana na matumizi ya afyuni za kutengenezwa (fentanyl na jamii zake) ikiwa ni ongezeko la asilimia **13** katika kipindi cha mwaka mmoja tu.

Mwaka huo huo kulitokea vifo vipatavyo **4,000** Nchini Canada ukilinganisha na vifo **300** vilivyotokea mwaka 2016 ambapo asilimia **69** vifo hivyo vilitokana na matumizi ya fentanyl na jamii zake.

Dawa ya fentanyl na jamii zake huuzwa kwenye mtandao zikinadiwa kuwa ni halali na mbadala wa dawa tiba zinazodhibitiwa (controlled drugs). Amerika ya Kaskazini ni kitovu cha biashara ya fentanyl na jamii zake ingawa kuna ushahidi kuwa tatizo la biashara ya dawa hii limeanza kuenea katika maeneo mengine duniani. Takwimu za ukamataji zilizoripotiwa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia uhalifu na dawa za kulevya (UNODC) zinaonesha kuwa mwaka 2013 nchi zilizokuwa na tatizo la fentanyl zilikuwa nne tu. Kufikia mwaka 2016 nchi zenye tatizo hilo zilifikia **12** na mwaka 2017 ziliongezeka na kufikia nchi **16.**

Cocaine

Kulikuwa na ongezeko la asilimia **25** la uzalishaji wa cocaine katika mwaka 2017 ikilinganishwa na mwaka 2016 ambapo tani **1,976** zilizalishwa. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa cocaine kwenye nchi ya Colombia ambayo ilizalisha asilimia **70** ya cocaine yote iliyopatikana duniani. Aidha, biashara ya cocaine imezidi kushamiri katika miaka ya hivi karibuni ambapo nchi zilizoripoti kukamata dawa hiyo ziliongezeka kutoka nchi **99** katika kipindi cha mwaka 1983 hadi 1987 na kufikia nchi **143** katika kipindi cha mwaka 2013 hadi 2017. Katika kipindi hicho inakadiriwa watu wapatao milioni **18.1** walitumia cocaine katika eneo la Amerika ya Kaskazini na Ulaya ya Kati na Magharibi.

Ukamataji wa cocaine uliongezeka kwa asilimia **70** duniani na uzalishaji wake uliongezeka kwa asilimia **50**. Mazingira haya yanaashiria kuwa kiwango kinachozalishwa ni kikubwa ikilinganishwa na kiasi kinachohitajika kwa matumizi. Katika mwaka 2017, mabara ya Amerika yaliongoza kwa ukamataji wa cocaine kwa asilimia **90** ya ukamataji wote. Colombia ambayo ni mzalishaji mkuu wa cocaine ilikamata asilimia **38** ya cocaine yote duniani kwa mwaka huo.

Cocaine imekuwa ikisafirishwa kutoka maeneo zalishaji kwenye milima ya Andes iliyopo Bara la Amerika ya Kusini kwenda kwenye masoko ya Amerika ya Kaskazini na Ulaya. Cocaine iliyokamatwa katika eneo la Amerika ya Kaskazini iliongezeka mara mbili kutoka tani **94** mwaka 2013 hadi tani **238** mwaka 2017. Ukamataji wa cocaine barani Ulaya uliongezeka mara mbili katika kipindi cha miaka mitano kutoka tani **65** mwaka 2013 hadi tani **141** mwaka 2017.

Dawa Mpya za Kulevya (NPS)

Dawa mpya za kulevya ni dawa zinazotengenezwa kwa kuiga kemikali zilizoko kwenye dawa za kulevya zinazodhibitiwa kimataifa ili kuficha uhalisia wa dawa hizo kukwepa mkono wa sheria. Dawa hizi zina madhara sawa au zaidi ya dawa zinazodhibitiwa na mikataba ya kimataifa. Dawa hizi hutengenezwa kutokana na dawa aina ya vichangamshi (ATS), Jamii ya bangi na vipumbaza (afyuni). Kumekuwa na ongezeko la uzalishaji haramu wa dawa mpya za kulevya hasa jamii za fentanyl na cannabinoids. Dawa mpya ya kwanza kuripotiwa ilikuwa mwaka 2009 na kufikia mwaka 2015 ziliripotiwa dawa mpya **15**. Dawa hizi ziliendelea kuongezeka hadi kufikia **46** mwaka 2017. Katika kipindi cha kati ya mwaka 2015 hadi 2017 kumekuwa na wastani wa dawa mpya za kulevya aina tofauti zaidi ya **800** zilizokuwa zikiingizwa sokoni kila mwaka.

Jitihada kubwa zimefanyika katika kuondoa mitandao ya siri ya kielektroniki inayotumiwa na wahalifu kuuza dawa za kulevya. Uondoaji huo ulifanikisha kupunguza kwa kiasi kikubwa biashara ya dawa za kulevya mitandaoni.

Methamphetamine

Methamphetamine ni aina ya dawa ya kulevya iliyo katika kundi la vichangamshi inayotengenezwa katika maabara bubu kwa kutumia kemikali bashirifu. Kiasi cha methamphetamine kilichokamatwa katika eneo la Asia ya Mashariki kiliongezeka mara nane zaidi na kufikia tani **82** ambayo ni sawa na asilimia **45** ya ukamataji wote duniani katika muongo mmoja kuanzia mwaka 2007 hadi 2017. Kiasi kikubwa cha methamphetamine kipatacho vidonge milioni **515** kilikamatwa nchini Thailand, ambacho ni kati

ya vidonge milioni **745** vilivyokamatwa katika eneo la Asia ya Mashariki. Aidha, takwimu za waraibu waliojitokeza kupata tiba zinaonesha kuwa methamphetamine ilikuwa ni dawa ya kulevya iliyoongoza kwa matumizi katika eneo la Asia ya Kusini na Mashariki.

Vileta njozi –"Hallucinogens"

Vileta njozi ni kundi la dawa za kulevya lenye sifa ya kuvuruga utendaji wa milango ya fahamu na kubadilisha mtazamo na uhalisia wa vitu. Dawa hizo ni pamoja na Bangi, LSD- Lysergic Acid Diethylamide na Ketamine. Ketamine ni dawa tiba yenye asili ya kulevya inayopatikana katika kundi la vileta njozi ambayo haidhibitiwi Kimataifa. Katika kipindi cha mwaka 2013 hadi 2017, asilimia **96** ya ketamine iliyokamatwa duniani ilitoka katika eneo la Asia ya Mashariki ambako inadhibitiwa. Hata hivyo, ketamine imeanza kuenea katika maeneo ya Ulaya, Amerika na Oceania. Amerika ya Kaskazini hususan nchi ya Marekani ilifanikiwa kukamata asilimia **88** ya vileta njozi (ukiiondoa ketamine) katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2017.

1.3 Upunguzaji Madhara yanayosababishwa na Matumizi ya Dawa za Kulevya

Maambukizi ya VVU, Homa ya Ini na Kifua Kikuu

Takribani watu milioni **11** duniani wanajidunga dawa mbalimbali za kulevya. Watu milioni **1.4** kati yao wana maambukizi ya VVU, watu milioni **5.6** wana ugonjwa wa homa ya ini aina C na watu milioni **1.2** wakiishi na VVU pamoja na virusi vya homa ya ini aina C. Asilimia **43** ya wajidunga wote duniani wanapatikana katika nchi za China, Urusi na Marekani.

Inakadiriwa kuwa katika kila wajidunga wanane, mmoja anaishi na maambukizi ya VVU. Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Maambukizi ya VVU na UKIMWI (UNAIDS) limekadiria kuwa mjidunga ana uwezekano mara **22** zaidi wa kuambukizwa VVU ikilinganishwa na watu wengine kwenye jamii. Eneo la Ulaya Mashariki na Asia ya Magharibi linaongoza kwa kuwa na wajidunga wengi wanaoishi na VVU wakifikia mara mbili zaidi ya wastani wa dunia.

Homa ya ini aina C

Maambukizi ya homa ya ini aina C ni makubwa mara nne zaidi ya VVU kwa wajidunga wa dawa za kulevya duniani. Inakadiriwa nusu ya wajidunga wanaofikia milioni **5.6** duniani wanaishi na virusi vya homa ya ini aina C. Hatahivyo, matibabu ya homa ya ini ni ghali na yanapatikana sehemu chache kwa kutumia dawa za kutibu virusi hivyo (Direct-acting antivirals). Vifo vinavyotokana na madhara ya matumizi ya dawa za kulevya hupunguza wastani wa umri wa kuishi kwa watumiaji wa dawa hizo. Inakadiriwa kuwa watu wapatao **585,000** walikufa kutokana na matumizi ya dawa hizo katika kipindi cha mwaka 2017. Nusu ya vifo hivyo vilitokanana na homa ya ini aina C ambayo husababisha ugonjwa wa ini "Liver Cirrhosis" na kansa ya ini. Licha ya kuwepo kwa vifo vingi vinavyotokana na matumizi ya dawa za kulevya duniani, sehemu kubwa ya waathirika hawapati huduma za matibabu. Inakadiriwa kuwa kati ya watu saba walioathirika na dawa hizo ni mmoja tu anayepata huduma za matibabu.

Matibabu Kwa Waraibu

Waathirika wengi wa matumizi ya afyuni pamoja na wajidunga wa dawa hizo waliohitaji tiba walipatikana zaidi katika maeneo ya Amerika ya Kaskazini na Asia ya Kusini na Mashariki. Watumiaji wa afyuni hasa heroin waliongoza katika kuhitaji tiba kwenye mabara ya Ulaya na Asia. Watumiaji wa cocaine ambao hutumia dawa nyingine za kulevya kama vile pombe na bangi, waliendelea kujiunga na huduma za matibabu katika Bara la Ulaya.

Miaka miwili iliyopita Nchi za Umoja wa Ulaya zilishuhudia ongezeko la watumiaji wa mara ya kwanza wa cocaine waliokwenda kwenye vituo vya matibabu wakiwa wameathiriwa na dawa hiyo. Robo tatu ya waathirika hao walitoka katika nchi za Italia, Hispania na Uingereza. Watumiaji wa bangi walioathirika kiafya kiasi cha kujiunga na huduma za tiba wameendelea kuongezeka duniani. Bara la Afrika liliongoza duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya watumiaji wa bangi wanaohitaji huduma za tiba.

1.4 Wanawake na matumizi ya dawa za kulevya

Wanawake hupata uraibu na madhara mengine yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya kwa haraka zaidi kuliko wanaume. Tafiti zinaonesha kuwa wanawake wengi duniani hutumia dawa tiba zenye asili ya kulevya (tranquillizers) kama vilevi. Hatahivyo, wanawake walioathirika na dawa hizo hupata uoga kujitokeza kwenye huduma za matibabu ya uraibu kutokana na unyanyapaa, ujauzito au kunapokuwa na matatizo ya kisheria. Matumizi ya dawa za kulevya kwa wajawazito husababisha athari kwa watoto wao na wanapojifungua suala la malezi huwa ni tatizo.

1.5 Wafungwa

Wafungwa ni kundi la kijamii ambalo liko katika hatari kubwa ya kupata madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya bila kuwa na huduma za afya za kutosha. Watumiaji wengi wa dawa za kulevya hujikuta wakifungwa kutokana na kujihusisha na uhalifu mbalimbali ili kupata fedha za kununua dawa za kulevya. Aidha, kutokana na mazingira magumu yaliyoko gerezani wafungwa wengi wanajiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya ili kukabiliana na mazingira hayo.

Takwimu chache zilizopatikana kwenye nchi zinazoendelea zinaonesha kuwa karibu nusu ya wafungwa wote walikuwa watumiaji wa dawa za kulevya kabla hawajaanza kutumikia vifungo vyao. Vilevile, tafiti hizo zilionesha kuwa idadi ya wanawake waliokuwa wanatumia dawa za kulevya ilikuwa kubwa kuliko wanaume. Kwani asilimia **51** ya wafungwa wanawake walikuwa wana uraibu wa dawa za kulevya mwaka mmoja kabla ya kifungo ikilinganishwa na asilimia **30** ya wanaume. Idadi hii ni kubwa ikilinganishwa na watumiaji wanawake na wanaume ambao hawajafungwa. Bangi ilikuwa ni dawa ya kulevya iliyoongoza kwa matumizi katika wafungwa hao. Asilimia **10** ya wafungwa walikuwa wanatumia dawa za jamii ya afyuni. Aidha, asilimia **10** ya wafungwa walitumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga.

Wafungwa wanaojidunga dawa za kulevya wanajiweka katika hatari kubwa ya kuambukizwa VVU na virusi vya homa ya ini aina C kuliko wanajamii wengine. Hii inatokana na uhaba wa sindano za kujidungia na hivyo sindano

moja kutumika na watu wengi hivyo kusababisha maambukizi makubwa ya virusi hivyo kati yao. Mapitio ya tafiti mbalimbali yanaonesha maambukizi ya VVU kati ya wafungwa wajidunga yalikuwa mara sita zaidi na homa ya ini aina C ikiwa mara nane zaidi ya wafungwa wasiojidunga.

Nchi **56** duniani ziliripoti kutoa huduma ya tiba ya methadone walau kwenye jela moja katika mwaka 2017. Huduma za udungaji salama kwa wafungwa ni chache sana, ambapo nchi **11** ziliripoti kutoa huduma hizo kwenye walau gereza moja. Huduma hiyo iliripotiwa kutokuwepo kabisa kwenye nchi **83.** Katika kupunguza maambukizi ya VVU na homa ya ini aina C huduma hizi mbili inabidi zitolewe kwa pamoja.

Kutokana na uwepo wa maambukizi makubwa ya VVU na homa ya ini aina C magerezani kuna umuhimu wa kuwa na huduma ya vipimo na matibabu ya maambukizi hayo. Ingawa maambukizi ya virusi vya homa ya ini aina C yalikuwa makubwa kuliko VVU huduma za upimaji na matibabu yake zilikuwa chache kuliko za VVU. Nchi **42** tu ziliripoti kutoa huduma ya upimaji homa ya ini aina C na nyingine **39** zikitoa matibabu yake. Ikilinganishwa na nchi **78** zilizoripoti kutoa huduma za upimaji VVU na nyingine **87** zikitoa matibabu yake.

SURA YA PILI

2 MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

2.1 Utangulizi

Sura ya pili inaelezea mikakati ya kudhibiti na kupambana na tatizo la dawa za kulevya Nchini ambayo ni kama ifuatavyo:

2.1.1 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya

Mkakati huu unalenga katika kupambana na uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya Nchini. Maeneo ya msingi ya mkakati huo ni Kukusanya na kuchambua taarifa za wafanyabiashara wa dawa za kulevya; Kukamata dawa za kulevya na wafanyabiashara wa dawa hizo; Kudhibiti uzalishaji wa dawa za kulevya (Kilimo na Uzalishaji); Kudhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya; na Kuandaa na kusimamia miongozo ya uteketezaji wa dawa za kulevya.

2.1.2 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya

Mkakati huu unalenga kutoa elimu kwa jamii kusudi isiingie katika biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Lengo ni kuhakikisha jamii haijihusishi na uzalishaji pamoja na biashara ya dawa hizo. Maeneo ya msingi ya mkakati huo ni Kutoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya katika jamii na Kuandaa miongozo ya uelimishaji kuhusu tatizo la dawa za kulevya

2.1.3 Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya

Mkakati huu unalenga katika kutoa tiba kwa jamii pamoja na kundi la watu waliaothirika na tatizo la matumizi ya dawa za kulevya. Lengo ni kuhakikisha jamii iliyoathirika na madhara ya matumizi ya dawa hizo inapata tiba na hivyo kupunguza madhara ya kiafya, kijamii na kiuchumi. Ni muhimu kufahamu kwamba uraibu wa dawa za kulevya ni tatizo la kiafya na huathiri watumiaji na jamii kwa ujumla, hivyo tiba ni muhimu ili kuwakinga watumiaji na jamii kwa pamoja. Maeneo ya msingi ya mkakati huo ni Kuratibu matibabu kwa waathirika wa dawa za kulevya; Kuandaa miongozo ya matibabu kwa waathirika wa dawa za kulevya; na Kufanya usimamizi

shirikishi katika vituo vinavyotoa huduma za tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya

2.1.4 Kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya

Mkakati huu wa nne unalenga katika kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa kwa kuwa tatizo la dawa za kulevya hasa biashara ya dawa za kulevya huendeshwa na mitandao ya kihalifu iliyopo nchi mbalimbali duniani. Vile vile, biashara ya dawa za kulevya huhusisha dawa zingine ambazo huzalishwa nje ya nchi hivyo, ni muhimu kuwa na mawasiliano miongoni mwa nchi mbalimbali. Maeneo ya msingi ya mkakati huu ni Kutekeleza mikataba na miongozo ya kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya; Kuhudhuria mikutano ya kisera na kisayansi kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya; Kubadilishana taarifa na mataifa mbalimbali kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya na Kutafuta na kushirikisha wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

SURA YA TATU

3 KUPUNGUZA UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA

3.1 Utangulizi

Sura hii imejikita katika jitihada zilizofanyika katika kutekeleza mkakati wa kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya nchini katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2019.

3.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya

Katika kipindi cha mwaka 2019, Tanzania iliendelea kukabiliwa na uwepo wa dawa za kulevya ambazo zimegawanyika katika makundi mawili za viwandani na mashambani.

Dawa za kulevya zinazopatikana Nchini huhusisha zinazozalishwa nchini na zile zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Dawa za kulevya zinazozalishwa nchini ni bangi, mirungi na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi ni pamoja na heroin, cocaine, mandrax, morphine na bangi iliyosindikwa.

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2019 kulikuwa na makosa **7,921** ya dawa za kulevya nchini. Kati ya hayo makosa **503** yalihusu dawa za kulevya za Viwandani na makosa **7,418** yalihusu dawa za kulevya za Mashambani. Aidha watuhumiwa **578** wa dawa za kulevya za Viwandani na watuhumiwa **10,326** wa dawa za kulevya za mashambani walikamatwa.

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2019 watuhumiwa, aina ya dawa za kulevya walizohusishwa nazo pamoja na kiasi cha dawa hizo kilichokamatwa ni kama ifuatavyo:

Bangi

Biashara ya bangi iliendelea kufanyika kwa mwaka 2019 na kukamatwa kwa tani **21.16** za dawa hiyo kiasi ambacho ni kidogo ikilinganishwa na tani **23.61** zilizokamatwa mwaka 2018. Hii inaonesha kuwa juhudi za kupambana na kudhibiti uzalishaji na usambazaji wa dawa hii una mafanikio. Pia, takwimu za ukamataji zinaonesha kuwa idadi ya watuhumiwa waliojihusisha na biashara ya bangi mwaka 2019 ilikuwa **8,865** ambayo ni ndogo zaidi ikilinganishwa na watuhumiwa **9,744** waliohusishwa na biashara ya dawa hiyo mwaka 2018.

Katika kipindi cha mwaka 2019 jumla ya Mashamba ya Bangi **31** yenye ukubwa wa Hekari **22** yakiwa na jumla ya miche ya bangi **1,997** yaliteketezwa na jumla ya watuhumiwa **29** walikamatwa kuhusiana na mashamba hayo. **(*Rejea Jedwali Na.1 na Kielelezo Na.1).***

Mirungi

Mwaka 2019 biashara ya mirungi iliendelea kufanyika ambapo jumla ya tani **9.07** za dawa hii zilikamatwa. Pia mwaka huo, kulikuwa na watuhumiwa **1,170** waliojihusisha na biashara hiyo, ambayo ni idadi ndogo ikilinganishwa na idadi ya watuhumiwa katika miaka mitano iliyopita **(*Rejea Jedwali Na.1 na Kielelezo Na.1).***

Jedwali Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2009-2019.

Mwaka	Bangi (Tani)	Mirungi (Tani)
2009	56.20	22.90
2010	4.03	3.69
2011	17.30	0.10
2012	48.70	6.22
2013	85.80	12.82
2014	81.30	15.74
2015	22.01	16.60
2016	68.23	21.64
2017	52.19	67.81
2018	24.30	8.96
2019	21.51	9.07

Kielelezo Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2009-2019.



Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2009-2019.



Kutokana na takwimu hapo juu, kiasi cha bangi kilichokamatwa kiliendelea kupungua kuanzia mwaka 2017 mpaka 2019 hii ni kutokana na kuimarika kwa jitihada za udhibiti. Halikadhalika, kiasi cha mirungi kwa mwaka 2019 kiliongezeka ukilinganisha na mwaka 2018 kutokana na kubainika kwa mtandao wa usafirishaji wa dawa hizo kutokea nchini Ethiopia kupitia Tanzania kwenda Ulaya, Marekani na Canada kwa njia ya Posta.

Jedwali Na. 2: Idadi ya watuhumiwa wa Bangi na Mirungi waliokamatwa kati ya mwaka 2009-2019

Mwaka	Idadi ya Watuhumiwa – Bangi	Idadi ya Watuhumi wa Mirungi
2009	3,382	365
2010	11	26
2011	39	100
2012	5,548	847
2013	1,547	581
2014	11,918	1,650
2015	13,275	1,780
2016	17,889	2,397
2017	11,528	1,797
2018	9,744	1,185
2019	8,865	1,170

Kielelezo Na. 3: Mwenendo wa idadi ya watuhumiwa waliokamatwa kwa kujihusisha na Bangi na Mirungi nchini kati ya Mwaka 2009 – 2019.



Kielelezo Namba 3 kinaonesha idadi ya watuhumiwa wa bangi na mirungi kwa mwaka 2019 imeendelea kupungua ikilinganishwa na miaka iliyopita huenda inatokana na watu wengi kuogopa kujihusisha na biashara hiyo kutokana na kuimarika kwa udhibiti.

Heroin

Mwaka 2019 jumla ya kilo **55.35** za heroin zilikamatwa nchini zikiwahusisha watuhumiwa **318**. (***Rejea Jedwali Na.3 na Kielelezo Na.4)***.

Cocaine

Mwaka 2019 biashara ya cocaine iliendelea kuwepo katika maeneo mbalimbali nchini. Hii inadhihirishwa na kukamatwa kwa kilo **10.34** za cocaine zikiwahusisha watuhumiwa **31.**

(***Rejea Jedwali Na.3 na Kielelezo Na.4)***.

Jedwali Na. 3: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2009-2019.

Mwaka	Kiasi cha Cocaine kilichokamatwa(Kg)	Kiasi cha Heroin kilichokamatwa (Kg)
2008	3.50	3.7
2009	4.39	9
2010	62.97	185.8
2011	128	264.26
2012	151	260
2013	4	36
2014	45	400
2015	17.79	64.75
2016	18.52	42.26
2017	4.14	185.56
2018	7.67	16.94
2019	10.34	55.35

Kielelezo Na. 4: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2009--2019.



Kielezo Na. 4 kinaonesha kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa kwa mwaka 2019 kimeongezeka ukilinganisha na mwaka 2018 hii ni kutokana kugundua mbinu mpya na ushirikiano wa kimataifa wa kukamata wafanyabiashara wakubwa ambao hukutwa na kiasi kikubwa cha dawa hizo.

Jedwali Na. 4: Idadi ya watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa nchini kati ya Mwaka 2009 - 2019.

Mwaka	Idadi ya Watuhumiwa wa Cocaine	Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin
2009	108	122
2010	8	15
2011	30	20
2012	138	400
2013	20	75
2014	351	584
2015	281	474
2016	263	716
2017	243	1005
2018	148	463
2019	31	318

Kielelezo Na. 5: Idadi ya watuhumiwa waliokamatwa wakijihusisha na Heroin na Cocaine kati ya Mwaka 2009 - 2019.



Kielelezo Na. 5 kinaonesha idadi ya watuhumiwa waliokamatwa na Heroin na Cocaine kwa mwaka 2019 wamepungua ukilinganisha na mwaka 2018 hii ni kutokana na Mamlaka kujikita katika ukamataji wa wafanyabiashara wakubwa wa dawa hizo.

Kielelezo Na. 6: Mwenendo wa idadi ya watuhumiwa waliokamatwa wakijihusisha na Heroin na Cocaine kati ya Mwaka 2009 - 2019.



Udhibiti wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya

Mamlaka iliendelea na udhibiti wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya kwa kutumia njia mbalimbali ambazo ni pamoja na kufanya ukaguzi, kutoa elimu, na kufuatilia mienendo ya miamala ya bidhaa hizo kupitia mifumo ya kielektroniki, na kushirikisha sekta binafsi katika udhibiti.

Udhibiti huo ulitekelezwa kwa mujibu wa Sheria mbalimbali za udhibiti ambazo ni pamoja na Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya namba 5 ya mwaka 2015 chini ya Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na dawa za Kulevya, Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali namba 3 ya mwaka

2003 (Udhibiti na Usimamizi) inayosimamiwa na Mkemia Mkuu wa Serikali na Sheria ya Chakula na Dawa namba moja ya mwaka 2003 chini ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

Mamlaka ilifanya ukaguzi katika maeneo **57** katika mikoa ya Dar es salaam, Mwanza, Kilimanjaro, Tanga na Mbeya. Maeneo yaliyokaguliwa ni pamoja na Kampuni zinazojihusisha na uingizaji, usambazaji na utumiaji wa kemikali bashirifu, maduka ya kuuza dawa tiba za binadamu zikiwemo dawa tiba zenye asili ya kulevya, kampuni zinazojihusisha na huduma za usafirishaji wa vifurushi ikiwemo Shirika la Posta nchini. Vilevile ukaguzi ulifanyika katika vituo vya mipaka vipatavyo nane ambavyo ni pamoja na Tarakea, Holili, Horohoro, Kabanga, Rusumo na Mutukula.

Katika kipindi cha Mwaka 2019, Mamlaka kwa kushirikiana na GCLA na TMDA ilifanya ukaguzi wa pamoja katika maeneo yanayojihusisha na kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Sambamba na ukaguzi huo, elimu ya udhibiti wa kemikali bashirifu ilitolewa kwa Maafisa wa Serikali waanaohusika na udhibiti pamoja na wadau zaidi ya wadau **650** kutoka kampuni mbalimbali zinazojihusisha na usafirishaji, usimamimizi wa kemikali, waingizaji na wasambazaji.

Matokeo ya kaguzi zilizofanyika ni kubainika kwa usafirishaji wa dawa za kulevya kupitia kampuni za kusafirisha vifurushi kwa kutumia majina bandia; Kuwepo kwa wadau wengi wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya ambao hawana ufahamu wa kutosha juu ya Sheria za Udhibiti; Kuongezeka kwa usafirishaji haramu wa dawa tiba zenye asili ya kulevya kama vile ketamine, pethidine na Diazepam hali inayopelekea uwezekano wa dawa hizi kuchepushwa kwenye masoko haramu; Utumiaji wa mabasi ya abiria kusafirisha kemikali, na dawa tiba zenye asili ya kulevya kupitia mipaka ya Namanga, Tarakea na Holili na Kuwepo kwa watu wanaotumia vibali vya kampuni zingine kufanya miamala ya kemikali bashirifu kutoka kampuni za usambazaji. Hatua hii inatoa mwanya wa dawa tiba zenye asili ya kulevya na kemikali bashirifu kuangukia mikononi mwa wahalifu.

Kwa kutumia mfumo wa kupashana taarifa ya Pre-Export Notification System (PEN) inayoratibiwa na Bodi ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (INCB), Mamlaka ilizuia uingizaji nchini zaidi ya tani **43.64** za kemikali bashirifu zilizokuwa ziingizwe nchini kinyume cha Sheria. Ukiukwaji wa Sheria hizo ni pamoja na kampuni hizo kutokuwa na vibali kutoka Mamlaka husika na kutumia majina ya kampuni zingine kuagiza kemikali bashirifu kutoka nje. Vilevile kwa kutumia mfumo wa kielekroniki mamlaka ilibaini mtandao wa usafirishaji dawa za kulevya aina ya mirungi kutoka nchini Ethiopia kupitia Tanzania na kisha kusafirishwa kwenda nchi za Uingereza, Marekani na Canada kupitia Shirika la Posta.

Kupitia Bodi ya Umoja wa Mataifa ya Kudhibiti dawa za Kulevya (INCB), Mamlaka inaratibu utekelezaji wa mradi wa ushirikishaji sekta binafsi kudhibiti uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Mamlaka kwa kushirikiana na Mamlaka zingine za udhibiti imetoa mafunzo kwa wadau **650** wanaojihusisha na kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya juu ya uelewa wa namna ya kutekeleza mradi huo. Aidha, Mamlaka imeandaa mifumo ya mawasiliano katika kubadilishana taarifa ikiwemo kuanzisha tovuti yenye tarifa za Udhibiti wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya (www.precursors.go.tz).

3.3 Uteketezaji wa Dawa za Kulevya

Dawa za kulevya zinazokamatwa huteketezwa kwa mujibu wa sheria kwa kushirikisha mamlaka mbalimbali za serikali baada ya hukumu kutolewa. Uteketezaji uliofanyika mwaka 2019 ulihusisha kilo **120.90** za heroin nakilo **70.96** za cocaine katika kiwanda cha Saruji cha Twiga kilichopo Wazo Hill jijini Dar es Salaam. Aidha, uteketezaji mwingine ulifanyika katika kiwanda cha Saruji jijini Mbeya ambapo kilo **1.65** za heroin na gramu **547.21** za cocaine ziliteketezwa.

Dawa za kulevya zikiteketezwa kwenye kiwanda cha saruji cha Twiga kilichopo Wazo Hill, jijini Dar es Salaam 12 Oktoba, 2019

3.4 Kesi za Dawa za Kulevya

Mwaka 2019, kesi **35** za dawa za kulevya zilimalizika katika Mahakama Kuu ya Tanzania. Mamlaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, ilifanikiwa kushinda kesi kubwa kadhaa. Miongoni mwa kesi hizo ni pamoja na iliyohusu kilo **63** za heroin kwenye Bahari ya Hindi ambapo watuhumiwa

walihukumiwa kifungo cha miaka **20** jela. Pia, katika kesi iliyohusisha raia **12** wa Iran wakiwa na jahazi waliokamatwa Februari 2018, Mahakama Kuu ya Tanzania iliwatia hatiani washitakiwa wote kwa kosa la kuwa na dawa ya kulevya aina ya bangi iliyosindikwa (hashish) pamoja na kufanya shughuli za uvuvi katika maji ya Tanzania Bara bila kibali. Washtakiwa wote kwa pamoja waliadhibiwa kulipa fidia ya Shilingi milioni **100** pamoja na kulipa faini ya shilingi milioni moja kila mmoja na jahazi lao kutaifishwa.

Aidha, kwa zaidi ya kesi **20** zilizoamuliwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania kwa mwaka 2019 asilimia 90 ya watuhumiwa wametiwa hatiani wakipewa adhabu ya kifungo cha kuanzia miaka **20** mpaka kifungo cha maisha gerezani kwa makosa mbalimbali ya kujihusisha na dawa za kulevya. Kwa Mahakama za chini jumla watuhumiwa **343** walitiwa hatiani, **65** waliachiwa huru na kesi **1,378** bado zipo katika hatua ya usikilizwaji Mahakamani.

Kutokana na taarifa ya kesi za dawa za kulevya inavyoonesha hapo juu, kumekuwa na mafanikio makubwa katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya hapa nchini kwa mwaka 2019.

SURA YA NNE

4 KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA

4.1 Utangulizi

Sura ya nne inaelezea jitihada zilizofanyika katika kutekeleza nguzo ya pili katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini. Tukumbuke kuwa nguzo ya kwanza inayohusu mapambano ya kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya nchini imezungumziwa katika sura ya tatu. Hivyo, sura hii ni mwendelezo wa sura ya tatu ikielezea jitihada katika kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya kwa kutoa elimu kwa jamii isijihusishe kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya

Dawa za kulevya hasa bangi, heroin, mirungi, cocaine na dawa tiba zenye asili ya kulevya zimeendelea kutumika nchini. Hali hii inadhihirishwa na watumiaji wanaojitokeza kutafuta tiba katika vituo vya kutolea dawa ya methadone, vituo vya kutolea huduma za afya, nyumba za upataji nafuu na asasi za kiraia, huduma za utengemao zinazotoa huduma kwa waraibu wa dawa za kulevya na tafiti mbalimbali. Watumiaji wengi wa dawa za kulevya huanza katika umri mdogo hivyo kuathiri makuzi yao kimwili na kiakili. Uchunguzi uliofanywa na Mamlaka unaonesha baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika jiji la Dar es Salaam wamekuwa wakitumia na kuuza dawa za kulevya hasa bangi kwenye shule zilizo maeneo ya wakazi wengi. Pamoja na wanafunzi, makundi mengine ya kijamii hutumia dawa za kulevya wakiongozwa na vijana.

4.3 Sababu zinazochangia Matumizi ya Dawa za Kulevya.

Matumizi ya dawa za kulevya yameendelea kuwa changamoto katika jamii yetu hasa kwa vijana wenye umri kati ya miaka 14-24 wengi wao wameanza kujihusisha na matumizi hayo wakiwa katika shule za msingi na sekondari. Hali hii huchangiwa hasa na sababu mbalimbali za kifamilia, kijamii na kiuchumi ambapo vijana wengi huanza kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya.

Miongoni mwa sababu hizo ni msukumo rika na kufuata mikumbo, ambapo baadhi ya vijana hupata kurubuniwa na kushawishiwa na vijana wenzao wanaotumia dawa hizo. Tatizo hili huwapata mara nyingi vijana wenye malezi duni, wenye mazingira magumu na hatarishi ya kuishi kama vile migodini na watoto wa mitaani. Makundi haya hujitokeza sana katika jamii kutokana na sababu mbalimbali za kifamilia ikiwemo kusambaratika kwa familia, malezi mabaya ya wazazi kwa watoto pamoja na umaskini. Vilevile, hali ya baadhi ya watoto kuishi na ndugu, rafiki, mpenzi au mwenza ambaye anajihusisha na dawa za kulevya huchangia katika kuanza matumizi hayo.

Urahisi na upatikanaji dawa za kulevya kama vile bangi na mirungi ambazo hutokana na mimea inayostawi sana katika maeneo mbalimbali nchini, zimekuwa kishawishi kikubwa kwa vijana wanaotoka maeneo hayo kujiingiza katika utumiaji wa dawa hizo. Aidha, ukosefu wa stadi za maisha na elimu ya kujitegemea kwa vijana pamoja na ukosefu wa ajira vimechangia kwa baadhi ya vijana kuingia katika matumizi hayo. Baadhi ya waathirika wa dawa hizo wameingia katika matumizi hayo kutokana na magonjwa ya akili kama vile saikosisi (kuchanganyikiwa) msongo wa mawazo, sonona na kihoro wamekuwa wakitumia dawa za kulevya kama njia ya kustahimili magonjwa hayo. Vilevile, kuongezeka kwa teknolojia za kisasa, utandawazi na mitandao ya kijamii vimechangia sana kwenye mmomonyoko wa maadili kwa vijana kwa kuiga maisha, mitindo, mila na desturi za kigeni ikiwemo kuingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

4.4 Madhara ya Dawa za Kulevya

Matumizi na biashara ya dawa za kulevya vimeendelea kuleta madhara ya kiafya, kijamii, kiuchumi, kisiasa na kimazingira.

Kiafya

Matumizi ya dawa za kulevya husababisha magonjwa mbalimbali yakiwemo ya akili, uraibu, moyo, ini na mapafu. Matumizi hayo pia huchangia kuenea kwa maambukizi ya VVU, virusi vya homa ya ini na kifua kikuu miongoni mwa watumiaji na jamii kwa ujumla. Aidha, matumizi hayo yanaweza kufanya mishipa ya damu kusinyaa na inapotokea hali hiyo kwenye ubongo husababisha shinikizo la damu na kiharusi. Aidha, dawa za kulevya

hupunguza kumbukumbu, uwezo wa kufikiri na kufanya maamuzi sahihi. Matumizi ya kiwango kikubwa cha dawa za kulevya kuliko alichozoea mtumiaji, husababisha vifo vya ghafla hasa kwa wajidunga.

Watumiaji wa dawa za kulevya hasa wanawake wajawazito wamekuwa wakijifungua watoto wenye uraibu wa dawa za kulevya na waliodumaa kimwili na kiakili. Madhara mengine ya kiafya ni pamoja na saratani, kupunguza nguvu za kiume, sonona, kukosa usingizi, kukosa hamu ya kula, kuoza meno, vidonda kwenye mfumo wa chakula na mara nyingine vifo. Kwa ujumla matumizi ya dawa za kulevya hupunguza umri wa kuishi wa mtumiaji kutokana na maradhi, uhalifu au kuzidisha dawa anayotumia.

Kijamii

Matumizi ya dawa za kulevya husababisha kukithiri kwa vitendo vya kihalifu katika jamii kama wizi, ukahaba, utapeli na uporaji ambayo hufanyika ili kupata fedha za kununulia dawa hizo. Kwa wafanyabiashara wa dawa za kulevya hulinda biashara zao kwa kutoa rushwa kubwa hivyo kuzuia kufikishwa kwenye vyombo vya dola au vyombo hivyo kutotenda haki, hali inayosababisha tatizo la dawa za kulevya kuongezeka kwenye jamii. Wafanyabiashara wa dawa za kulevya huendesha magenge ya utekaji, mapigano na mauaji na kuifanya jamii kuishi kwa woga. Wauzaji wa dawa za kulevya wana kawaida ya kujihusisha na biashara nyingine haramu kama biashara ya binadamu ambapo huwaweka watu rehani (bondi), silaha za magendo, meno ya tembo, nk. Wafanyabiashara wa dawa za kulevya huweza kuvuruga usalama kwa kufadhili vita na ugaidi.

Mahusiano katika familia huvurugika ambapo ndoa huvunjika na watoto hutelekezwa na iwapo mtoto ni mtumiaji huacha au hufukuzwa shule, hufukuzwa nyumbani na kuishi kwenye magheto ambako hubobea kwenye matumizi ya dawa za kulevya na uhalifu. Kuongezeka kwa maambukizi ya VVU, homa ya ini na kifua kikuu katika jamii kutoka kwa watumiaji ambao huwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya maradhi hayo. Unyanyapaa kwa watumiaji husababisha wakose haki zao za kifamilia na kijamii na hata pale wanapoacha matumizi ya dawa za kulevya familia zao au waajiri hushindwa kuwakubali. Pia matumizi ya dawa za kulevya husababisha ajali zinazozuilika zinazoleta ulemavu, vifo na uharibifu wa mali na miundombinu.

Kiuchumi

Matumizi ya dawa za kulevya hudhoofisha afya za watumiaji na kupunguza ufanisi wao kazini au kwenye masomo na wale ambao hawana ajira kutoweza kupata ajira kutokana na kuathiriwa na dawa za kulevya (Uraibu) hivyo kuleta umaskini kwake mtumiaji, jamii yake na taifa kwa ujumla.

Biashara wa dawa za kulevya husababisha mfumuko wa bei na kuondoa mizania ya ushindani wa kibiashara kwa kuwa uwezo wa kununua bidhaa kwa bei ya juu kuliko bei ya kawaida ya soko hivyo kuwakosesha wengine fursa na kuongeza pengo la kipato kati yao na wananchi wa kawaida hali inayosababisha umaskini.

Dawa za kulevya huambatana na utakatishaji wa fedha haramu zinazotokana na biashara hiyo ambapo madhara yake ni pamoja na kuhamisha nguvu ya kifedha kutoka kwenye Serikali, masoko na wananchi na kwenda kwa wahalifu ambao ni wafanyabiashara wa dawa za kulevya. Vilevile, utakatishaji fedha huathiri taasisi za kifedha kama vile benki pale mhalifu anapoamua kutoa fedha zake kwa mkupuo ambapo mara nyingi huwa ni kiasi kikubwa na hivyo kuiacha taasisi ya kifedha ikiyumba na kuzorotesha ukuaji wa uchumi.

Jamii na Serikali huingia gharama zisizo za lazima kwa ajili ya ukamataji, matibabu ya waraibu, kutoa elimu ya kupunguza matumizi ya dawa za kulevya na kutunza wafungwa gerezani badala ya kuelekeza rasilimali hizo kwenye maendeleo hivyo kurudisha nyuma jitihada za kukuza uchumi wa nchi.

Kisiasa

Kutokana na uwezo wao mkubwa wa kifedha wafanyabiashara wa dawa za kulevya huweza kujiingiza katika shughuli za kisiasa na hivyo kuwepo na uwezekano wa nchi kupata viongozi wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya. Pia, wafanyabiashara hao wanaweza kufadhili chaguzi au kuwaondoa viongozi waliochaguliwa kidemokrasia na kuwaweka watu wao madarakani ili kulinda biashara na maslahi yao. Hali hii huweza kuathiri mustakabali wa nchi kwa kutawaliwa na magenge ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya na jamii ya waraibu wa dawa hizo.

Kimazingira

Kilimo cha bangi na mirungi hufanyika katika maeneo yasiyofikika kirahisi kama vile kwenye milima, misitu na kwenye vyanzo vya maji na hivyo kusababisha kukauka kwa vyanzo vya maji, ukame, mmomonyoko wa ardhi na kutoweka kwa baadhi ya viumbe hai na uoto wa asili. Uharibifu huu umejidhihirisha katika baadhi ya safu za milima ya Uluguru, Usambara, Udzungwa, Upare na maeneo ya Arumeru. Aidha, wajidunga wa dawa za kulevya wamekuwa wakitupa ovyo mabomba ya sindano yaliyotumika kwenye majalala, vichochoro, viwanja vya michezo, fukwe na vituo vya daladala hivyo kuiweka jamii kwenye hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa yanayoambukiza kwa njia ya damu kama VVU na homa ya ini.

4.5 Kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na wadau wengine hutoa elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya katika makundi mbalimbali ya kijamii ili jamii isijihusishe na matumizi ya dawa hizo. Elimu hii hutolewa kupitia vyombo vya habari, machapisho, maadhimisho ya kitaifa, semina na makongamano.

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2019, Mamlaka ilitoa elimu kwenye Maadhimisho ya Siku ya Kupambana na Dawa za Kulevya Duniani kitaifa. Katika maadhimisho hayo elimu ilitolewa katika maeneo yaliyokithiri kwa matumizi na biashara ya dawa za kulevya katika Jiji la Tanga, ambako vijana takribani **180** waliopo katika mazingira hatarishi ya kujihusisha na dawa za kulevya walipata elimu ya madhara ya dawa za kulevya na kwa wale waliopata uraibu wa dawa hizo walihamasishwa kujiunga na tiba. Aidha, elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya iliendelea kutolewa kwa wakazi wa Tanga katika viwanja vya Tangamano ambapo maadhimisho hayo yalifanyika.

Maandamano ya kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kupinga Dawa za Kulevya Duniani, Kitaifa uwanja wa Tangamano mkoani Tanga, Juni 26,2019

Mamlaka ilishiriki kutoa elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya katika Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Wakulima Kitaifa maarufu kama "Nanenane", Bariadi mkoani Simiyu, mwezi Agosti, 2019. Mamlaka ilikuwa na banda la uelimishaji lililonufaisha umma wa Kanda ya Ziwa Mashariki inayohusisha mikoa ya Simiyu, Mara na Shinyanga. Banda la Mamlaka liliweza kupata takribani watu **1,200** waliopatiwa elimu ya kuwaepusha na matumizi na biashara ya dawa za kulevya na kwa wale waliopata uraibu walielekezwa katika vituo vya kutolea huduma za tiba.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ina ujumbe wa kudumu kuhusu dawa za kulevya katika mbio za Mwenge ambao husambazwa nchi nzima ukihamasisha wananchi kujiepusha na matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Mamlaka pia imekuwa ikifanya uelimishaji katika Maadhimisho ya Wiki ya Vijana iliyoadhimishwa kitaifa Mkoani

Lindi, Oktoba, 2019. Kupitia banda la Mamlaka wageni takriban **850** walipatiwa elimu ya dawa za kulevya.

Katika kukabiliana na tatizo la matumizi ya dawa za kulevya lililoshika kasi katika shule za msingi na sekondari nchini, Mamlaka pamoja na asasi zinazotoa elimu ya dawa za kulevya zilitoa elimu kwa wanafunzi wapatao **26,458** katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Pamoja na kupatiwa elimu hiyo wanafunzi hao walihamasishwa kuanzisha klabu za kupinga dawa za kulevya kwenye shule zao na kwenye baadhi ya shule kuimarisha zilizopo.

Asasi zilizoshirikiana na Mamlaka kutoa elimu ya dawa za kulevya shuleni ni NURGET Development Tanzania, Youth Empowerment Aid Organizantion, Harakati Networking Organization, Community Oriented Development Action (CODATz), Guluka Kwalala Youth Environment group, Youth Counseling and Rehabilitation Centre (YCRC), Youth Achievement Village in Tanzania (YAVT), Dynasty Basketball Centre, Tanzania Organization of Good Templars (T-OGT), Gift of Hope Foundation, Kim Hope Foundation, Next generation Keepers, Kimara Peer Educators and health Promoters Trust Fund, Harakati Networking Organization na Kibwena Community Development (KICODE). Asasi hizi pia zilitoa elimu ya dawa za kulevya kupitia vyombo vya habari, makanisani na mitaani.

Vilevile, Mamlaka ilitoa elimu ya dawa za kulevya kwa wanachuo waliojiunga na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Jijini Dar es Salaam katika ngazi ya cheti na stashahada wapatao **200**. Elimu ililenga kuwapatia ufahamu wa kujiepusha na matumizi na biashara ya dawa za kulevya yaliyoshika kasi kwenye vyuo mbalimbali nchini.

Vilevile, elimu ya dawa za kulevya ilitolewa kwa wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Tanga. Mamlaka kwa kushirikiana na BASATA na TACAIDS, ilifanya kongamano la utoaji wa elimu ya VVU na Dawa za kulevya kwa wasanii **850** katika kipindi cha mwaka 2019 Jijini Dar es salaam.

SURA YA TANO

5 KUPUNGUZA MADHARA YANAYOTOKANA NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

5.1 Utangulizi

Upunguzaji wa madhara yanayosababishwa na matumizi na biashara ya dawa za kulevya ni nguzo ya tatu kati ya nguzo kuu nne za kudhibiti na kupambana na tatizo hilo. Nguzo hii inalenga kupunguza madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya ikiwemo uraibu, maambukizi ya VVU, homa ya Ini, Kifua Kikuu, Magonjwa ya afya ya akili na kupunguza usugu kwa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI na kifua kikuu pamoja na unyanyapaa kwa watumiaji wa dawa za kulevya. Hivyo kupitia nguzo hii waathirika wa dawa za kulevya wanapata fursa ya kupata tiba ya uraibu na matatizo mengine ya kiafya, sambamba na kuwaunganisha katika jamii na familia zao.

Mamlaka kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kutoa elimu na tiba kwa waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya ili kupunguza madhara kwenye jamii. Aidha, Mamlaka imekuwa ikifanya usimamizi shirikishi kwa vituo vya kutolea huduma za afya, asasi za kiraia na vikundi mbalimbali vinavyojihusisha na mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

5.2 Tiba ya Methadone

Huduma ya methadone ni tiba maalum kwa ajili ya kuwatibu waraibu wa dawa za kulevya aina ya afyuni pamoja na matatizo mengine ya afya yanayoambatana na uraibu wa dawa hizo. Tiba hii imegawanyika katika sehemu mbili ambapo ni huduma katika jamii na huduma katika vituo vya afya. Huduma katika jamii hutolewa na asasi za kiraia kwa kuwatafuta na kuwandaa waraibu kwenda kwenye vituo vya tiba. Uandaaji wa waraibu huanza kwa kupita kwenye vijiwe vya waathirika wa dawa za kulevya na kuwapatia huduma ya unasihi (counseling) na kuwaunganisha na familia zao. Aidha, waraibu hao hupatiwa elimu ya dawa za kulevya na kupewa rufaa ya kwenda kwenye tiba ya methadone na huduma mbalimbali za afya.

Jedwali Na. 5: Idadi ya waraibu waliohudumiwa na asasi za kiraia

Na.	Asasi	Waraibu	Me	Ke
1.	Methadone Family Against Drugs Abuse - MEFADA (DSM)	241	228	13
2.	Methadone Family Against Drugs Abuse - MEFADA (Dodoma)	117	114	3
3.	Youth Community Rehabilitation- YCR (Dodoma)	117	115	2
4.	Youth Volunteers against Risky Behaviors – YOVARIBE (DSM)	269	221	9
5.	Youth Volunteers against Risky Behaviors -YOVARIBE (Dodoma)	111	106	5
	Jumla	**855**	**784**	**32**

Baada ya maandalizi ya waraibu katika jamii na asasi husika, hupelekwa kwenye vituo vya afya vya kutolea huduma ya methadone. Huduma hii inahusisha tiba ya uraibu wa dawa za jamii ya afyuni hasa heroin pamoja na magonjwa shirikishi kama vile VVU, Homa ya Ini na Kifua Kikuu. Vilevile, waraibu katika vituo hivyo hupata tiba ya magonjwa ya zinaa na elimu ya uzazi, magonjwa ya akili pamoja na magonjwa yoyote ambayo yangeweza kutibiwa katika kituo chochote cha afya cha Serikali.

Hadi Desemba, 2019 Serikali ilifanikiwa kufungua jumla ya vituo sita vya kutolea huduma ya Dawa ya Methadone nchini. Vituo vitatu viko katika mkoa wa Dar es Salaam katika hospitali za rufaa za mikoa za Mwananyamala, Temeke na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Vituo vingine vitatu vipo katika mikoa ya Mwanza, Mbeya na Dodoma. Vituo hivyo kwa pamoja vimesajili waraibu wapatao **7,638**, kati yao wanaume ni **7,167** na wanawake ni **471** kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa sasa, wastani wa matumizi ya dawa ya methadone nchini ni kilogramu **300** kwa mwaka.

Faida ya Huduma za Methadone

Huduma ya tiba ya methadone ina faida zifuatazo: -

- Kupunguza uraibu na madhara yatokanayo na dawa za kulevya;
- Waraibu wa dawa za kulevya kupata tiba za magonjwa mengine yanayoambatana na matumizi ya dawa za kulevya kama vile UKIMWI, Kifua Kikuu na magonjwa ya ngono;
- Kupunguza vitendo vya uhalifu na hivyo kupunguza mrundikano wa watuhumiwa katika vituo vya Polisi na Magereza;
- Kupunguza uwezekano wa kutokea kwa usugu wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI na vimelea vya Kifua Kikuu;
- Kupata fursa ya tiba ya kwa waathirika wa dawa za kulevya;
- Kupunguza unyanyapaa kwa waathirika wa dawa za kulevya;
- Kurudisha ufahamu kwa waathirika wa dawa za kulevya na kuwafanya kujihusisha na shughuli mbalimbali za uzalishaji. Hatua hii huboresha ustawi wa maisha yao na hivyo kuwafanya raia wema na wenye kukubalika katika jamii;
- Kupunguza vifo vitokanavyo na kuzidisha kiwango cha matumizi ya dawa za kulevya; na
- Kupunguza mzunguko wa fedha haramu kwa wafanyabiashara wa dawa za kulevya.

5.3 Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses)

Nyumba za upataji nafuu ni nyumba maalum ambamo waathirika wa dawa za kulevya walioamua kuachana na matumizi ya dawa za kulevya hupatiwa msaada wa kuachana na matumizi ya dawa hizo kwa kutumia hatua 12 za upataji nafuu. Nyumba hizi huendeshwa na Asasi za Kiraia au watu binafsi kwa kufuata Mwongozo wa Serikali wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Nyumba za Upataji Nafuu wa Tanzania Bara. Katika kipindi cha mwaka 2019 huduma ya upataji nafuu iliendelea kutolewa. Nyumba hizi ziliweza kuwahudumia waraibu **3,663** ikiwa wanaume ni **3,609** na wanawake ni **74.**

Jedwali Na. 6: Waraibu Waliopata Huduma katika nyumba za upataji nafuu kwa mwaka 2019

No.	Asasi	Waraibu	Me	Ke
1.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (DSM)	122	122	-
2.	Changamoto ni Matumaini (DSM)	95	95	-
3.	Drug Free Tanzania –The Right Way Recovery House (DSM)	56	56	-
4.	Drug Free Tanzania –The Ties that Bind us Recovery Center (DSM)	51	51	-
5.	People with Drug Dependence and Relief Foundation (PEDDEREF) (DSM)	122	94	28
6.	People with Drug Dependence and Relief Foundation (PEDDEREF) (Dodoma)	32	32	-
7.	Kipepeo Foundation – South Beach Sober House (DSM)	85	85	-
8.	Sobriety Forever Rehabilitation Centre (Kagera)	17	17	-
9.	Courage on Recovery Foundation (Tanga)	127	127	-
10.	Life and Hope Rehabilitation Organization (Pwani)	170	150	20
11.	Kilimanjaro New Vision and Sobriety (Kilimanjaro)	137	122	15
12.	Tanzania Sobriety and Rehabilitation Organization (Dodoma)	35	35	-
13.	Tanga Drug Free Organization (Tanga)	68	68	-
14.	Pillimisanah Foundation (DSM)	2,257	2,257	-
15.	The Light of Miracle Organization – (Women's Hope Rehabilitation (Pwani)	11	-	11
16.	Gift of Hope Foundation (Tanga)	57	57	-
17.	New Vision of Life Society Sober House (DSM)	110	110	-
18.	Kipepeo Foundation – Free at Last Sober House (Morogoro)	55	55	
19.	Stay Clean Foundation- Goodwill Recovery Centre (Kilimanjaro)	61	61	-
20.	Tabora Sober House (Tabora)	15	15	-
	Jumla	**3,683**	**3,609**	**74**

SURA YA SITA

6 USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA KATIKA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

6.1 Utangulizi

Tatizo la dawa za kulevya ni suala mtambuka ambalo linahitaji ushirikiano na suluhisho la pamoja kuanzia ngazi ya kimataifa na kikanda, kama moja ya mikakati mikuu ya kupambana na tatizo hilo. Kutokana na umuhimu wa mkakati wa kuimarisha ushirikiano katika kudhibiti na kupambana na tatizo hili, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani (UNODC) kupitia Andiko lake la mwaka 2009 la Sera na Mpango Mkakati wa Udhibiti wa Dawa za Kulevya Duniani limeweka mkakati wa ushirikiano kama mkakati wa nne wa kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya. Serikali ya Tanzania kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imefanikiwa kuingiza mkakati huo kama moja ya mikakati minne ya kupambana na dawa za kulevya kwa kuimarisha ushirikiano katika nyanja zote tajwa.

6.2 Ushirikiano wa Kimataifa

Serikali ya Tanzania imekuwa ikifanya kazi katika ngazi ya kimataifa kwa kushirikiana kwa karibu na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) lenye makao makuu jijini Vienna, Austria. Ushirikiano huo umedhihirika katika kufuata miongozo na mikataba ya kimataifa ya kisera na kimkakati dhidi ya tatizo la dawa za kulevya. Tanzania imekuwa ikitekeleza mikataba yote ya kimataifa kuanzia mkataba wa 1961, 1971 na 1988 katika udhibiti wa Dawa za Kulevya. Aidha, Nchi yetu inatekeleza mkataba wa Makosa ya Jinai yanayovuka mipaka (Transnational Organized Crime TOC) wa mwaka 2000 unaozungumzia uhalifu wa kupangwa ambapo tatizo la dawa za kulevya limezungumziwa pia.

Aidha, nchi yetu inatekeleza kwa vitendo Mpango Mkakati wa Umoja wa Mataifa wa Kisera wa mwaka 2009 kupambana na tatizo la Dawa za kulevya ujulikanao kama Azimio la Kisera la Mpango kazi wa mwaka 2009 (Political Declaration and Plan of Action of 2009). Mpango huo unazungumzia umuhimu wa kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya kwa kutumia mikakati yenye uwiano sawa (balanced approach) ya mfumo jinai na

umuhimu wa kinga na tiba. Tanzania imepokea waraka kutoka Umoja wa Mataifa ambao unatoa dira (road map) ya utekelezaji wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Vilevile, nchi yetu imekuwa ikishiriki katika mikutano mbalimbali inayoratibiwa na Shirika la UNODC juu ya udhibiti wa dawa za kulevya. Mikutano hiyo ni mkutano wa Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Duniani (CND), and ministerial segment meetings. Vilevile, UNODC wamekuwa mstari wa mbele kwa kutoa mafunzo kwa maafisa wa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na Taasisi nyingine zinazoshiriki katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya ambapo kwa mwaka 2019 maofisa 40 walipata mafunzo kutoka katika shirika hilo.

Shirika hilo pia lina bodi mbalimbali ambazo zimekuwa zinashirikiana na Serikali yetu kama vile Bodi ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (International Narcotic Control Board (INCB). Bodi hii ni muhimu na ipo chini ya UNODC ambapo hushughulika na suala zima la udhibiti wa dawa za kulevya, dawa tiba zenye asili ya kulevya pamoja na kemikali bashirifu. Bodi hii imekuwa na kipaumbele kwa kutoa mafunzo na misaada ya kitaalam (technical support) kwa maofisa juu ya udhibiti dawa na kemikali hizo. Pia, Bodi imeweka mfumo wa pamoja wa kubadilishana taarifa na Mamlaka juu ya kemikali bashirifu zinazoingia nchini kwa ajili ya ufutiliaji. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na INCB imefanikiwa kufuatilia usafirishaji haramu wa kemikali bashirifu kwa kutumia mfumo wa kupashana taarifa ya Pre –Export Notification System (PEN) ambapo Mamlaka ilifanikiwa kuzuia uingizaji haramu wa kemikali bashirifu zaidi ya kilo **43,638** zilizokuwa ziingizwe nchini kinyume cha Sheria.

6.3 Ushirikiano wa Kikanda

Serikali ya Tanzania imekuwa ikipambana na tatizo la dawa za kulevya katika ngazi ya kanda kwa kushirikiana kwa karibu na Umoja wa Afrika (AU) wenye makao makuu jijini Addis Ababa, Ethiopia. Umoja huo umekuwa ukitoa miongozo ya kisera na kimkakati katika kupambana na tatizo hilo. Vilevile, nchi yetu imekuwa ikishiriki katika Mkutano wa kila mwaka wa Viongozi wa Vyombo vinavyopambana na dawa za kulevya Afrika ujulikanao kama HONLEA Afrika. Lengo la mkutano huo wa kila mwaka ni kubadilishana uzoefu, kushirikiana katika upatikanaji wa taarifa pamoja na kupanga mikakati ya pamoja katika udhibiti wa tatizo la dawa za kulevya barani Afrika. Nchi yetu ilishiriki pia katika mkutano wa mwaka 2019 wa HONLEA ambao ulifanyika jijini Port Louis, Mauritius.

Vilevile, nchi yetu imeingia mkataba na nchi ya Msumbiji na Afrika Kusini katika kufuatilia wafanyabiashara wakubwa wa dawa za kulevya kwa kubadilishana taarifa za kiintelijensia zinazohusu dawa za kulevya na uhalifu wa kupanga (transnational organized crime). Mikataba hii inaratibiwa na UNODC.

6.4 Ushirikiano na Taasisi nyingine za Kimataifa

Serikali imekuwa ikishirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa katika kupambana na kudhibiti tatizo la dawa za kulevya katika maeneo makubwa matatu ya kimkakati ambayo ni ukamataji, utoaji wa elimu, kinga na tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya. Baadhi ya wadau wakubwa katika mashirikiano hayo katika upande wa ukamataji wa wauzaji na wasambazaji wa dawa za kulevya ni pamoja na Drug Enforcement Adminstration (DEA) ya Marekani, National Crime Agency (NCA) ya Uingereza, Naval Criminal Investigative Services (NCIS) ya Marekani, Combined Maritime Force ya Canada, Royal Canadian Mounted Police-CANADA (RCMP), EU-ACT na Indian Ocean Forum on Maritime Crime. Kutokana na ushirikano huo, Mamlaka imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuzuia uingizaji wa dawa za kulevya kupitia milango ya bahari pamoja na kwenda kufanya upekuzi wa baadhi ya meli katika bahari kuu kulingana na Sheria za Kimataifa.

Taasisi hizo zimekuwa mstari wa mbele katika kutoa mafunzo ya ndani na nje ya nchi kwa maofisa wa DCEA ya namna bora ya kudhibiti dawa za kulevya pamoja na kupatiwa vitendea kazi mbalimbali vya uchunguzi na utambuzi. Pia, Taasisi hizo zimeiwezesha Mamlaka kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kimataifa ya kujadili mbinu na njia bora za kupambana na dawa za kulevya. Ushirikiano huu umewezesha kubadilishana taarifa nyingi za kiintelijensia na kufanikisha kuharibu mitandao mikubwa ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya.

Vilevile, taasisi za nje za CDC, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (GF) na EU-ACT zimekuwa mstari wa mbele katika kutoa mafunzo ya upunguzaji uhitaji wa dawa za kulevya pamoja na tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya. Aidha, taasisi hizi kwa kushirikiana na Mamlaka zimeweza kuratibu mafunzo kwa watoa huduma wa afya kuhusu uraibu na tiba ya methadone kwa waathirika wa dawa za kulevya nchini.

6.5 Ushirikiano wa Wadau Nchini

Mamlaka imeshirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama nchini katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya hasa katika nyanja ya uzalishaji, usambazaji na uuzaji. Ushirikiano huo umeimarishwa pia katika mapambano dhidi ya uhalifu wa kupangwa kama vile ugaidi, utakatishaji fedha, usafirishaji haramu wa binadamu, uuzaji haramu wa silaha na utoroshaji wa nyara za Serikali kwa kuwa makosa hayo yanaendana na tatizo la biashara haramu ya dawa za kulevya. Taasisi hizo ni Polisi, Magereza, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Usalama wa Taifa, Uhamiaji, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Mamlaka ya Anga, Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Baraza la Famasia na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

Kwa upande wa upunguzaji wa uhitaji wa dawa za kulevya na uimarishaji wa tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya, Mamlaka imeshirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia katika utekelezaji wake. Juhudi zimeelekezwa zaidi katika utoaji wa elimu kupitia vilabu vya kupinga dawa za kulevya mashuleni pamoja na kuimarisha upanuaji wa huduma za tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya. Pia, Serikali kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeweza kushirikiana na taasisi mbalimbali zisizo za kiserikali nchini katika kuzuia uhitaji wa dawa za kulevya pamoja na tiba kwa waathirika wa dawa hizo. Mamlaka imeweza kutengeneza miongozo ya utendaji kazi wa taasisi hizo pamoja na kufanya usimamizi shirikishi ili kuboresha ubora wa utoaji huduma wa taasisi hizo. Baadhi ya Taasisi hizo ni MDH, TAYOA, MKIKUTE, T-OGT, YOVARIBE, MEFADA na YCR.

Vilevile, Mamlaka imeweza kutoa msaada kwa baadhi ya taasisi hizo zisizo za Kiserikali kwa kuwapatia vifaa vya ofisi kama vile kompyuta, pikipiki na misaada ya kifedha. Misaada hiyo imekuwa ikitolewa kupitia vyanzo vya ndani na nje ili kuimarisha zaidi harakati za taasisi hizo za kupambana na tatizo la dawa za kulevya nchini.

SURA YA SABA

7 CHANGAMOTO NA MIPANGO YA BAADAYE

7.1 Utangulizi

Sura hii imeainisha changamoto na Mipango ya baadaye ambayo Serikali imejiwekea katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini.

7.2 Changamoto

1. Mashahidi kuogopa kutoa ushahidi mahakamani;
2. Uhaba wa vitendea kazi vya kufanyia upekuzi na mitambo ya utambuzi wa haraka wa dawa wakati wa operesheni kutambua dawa mpya zinazoingizwa sokoni;
3. Usalama mdogo wa maafisa na kutishiwa maisha na wahalifu wa dawa za kulevya;
4. Kuibuka kwa mbinu nyingi za kuficha dawa na kemikali bashirifu ikiwemo kutumia majina bandia ya bidhaa halali;
5. Ulegevu wa sheria juu ya udhibiti wa dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya Ketamine na Tramadol kulingana na kuongezeka kwa mwenendo wa matumizi haramu ya dawa hizo;
6. Utengenezaji wa dawa mpya za kulevya kwa kutumia kemikali bashirifu ili kukwepa sheria zilizopo; na

7.3 Mipango ya baadaye

1. Kuwapatia watumishi waliopo nyenzo na mafunzo ili wafanye kazi za udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya kwa ufanisi;
2. Kuingiza dawa tiba aina ya Ketamine na Tramadol kwenye udhibiti wa kitaifa kwa kufanya marekebisho ya sheria iliyopo na kuifanya kuwa dawa zinazodhibitiwa kitaifa;
3. Mamlaka iko katika hatua za mwisho kufungua vituo vingine vitatu vya huduma ya dawa ya methadone katika hospitali ya wilaya ya Bagamoyo, hospitali ya Rufaa ya Tumbi na hospitali ya Bombo mkoani Tanga; na

4. Mamlaka inatarajia kuwa na maabara ya sayansi jinai kwa ajili ya uchunguzi na utafiti wa dawa za kulevya, kemikali bashirifu, dawa tiba zenye asili ya kulevya pamoja na dawa mpya za kulevya (NPS).
5. Mamlaka inatarajia kuwa na mfumo wa ushirikishaji wadau (PPP) katika kudhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu na hivyo kupunguza matumizi ya rasilimali katika kupata taarifa za wahalifu kwa wakati.